**Learning by Ear – Elimu na Kazi**

**Elimu ya Chuo Kikuu- Hadithi ya Malaika/ Episode 03**

**Mwandishi: Njoki C. Muhoho**

**Mhariri: Maja Dreyer**

**Tafsiri: Eric Ponda**

| WAHUSIKA: | | |
|---|---|---|
| Mtangazaji | - | Mwanamume |
| Malaika | - | Msichana miaka19 |
| Muhadhiri | - | Miaka 48 hivi. |
| Daniel | - | Mvulana miaka 20 |
| Cindy | - | Msichana miaka 19 |

**<u>INTRO</u>**

**MUZIKI: UTANGULIZI**

**1. MTANGAZAJI :** Ni wakati mwengine tena tunapoungana kukuletea makala ya tatu ya "Learning by Ear" Noa bongo jenga maisha yako, tunazungumzia Elimu ya Chuo kikuu. Katika kipindi kilichotangulia, Malaika anakuta mambo si rahisi chuoni, anajipata akifanya kazi kupita kiasi. Rafiki yake Cindy, ambaye ni mkaazi mwenza chumbani, anajaribu kumpa muongozo kuhusu maisha chuoni. Malaika anagundua kuna mengi ya kujifunza nje ya

darasani. Hata hivyo bado anafahamu fika jukumu na wajibu wake kimasomo, asije aibisha kijiji chake.

**SCENE 1: DARASANI:**

**SFX: MAKALELE YA MEZA NA VITI VIKIVUTWA HUKU WANAFUNZI WAKINONG´ONEZANA.**

2. MUHADHIRI :… Si haraka hivyo….! Ni kazi!

3. WANAFUNZI : Wanaguma

4. MUHADHIRI : Someni sura ya 2, 3, 4 na 5. Jibu swali la 3 na 8. Majibu ya maswali hayo lisipungue maneno 2,000. Kazi hiyo iwe tayari tutakapokutana tena. Na mkumbuke matokeo ya kazi hii yatajumuishwa kwenye gredi zenu za mwisho.

5. WANAFUNZI : Wakiendelea kuguma.

**SFX: Makelele ya viti na meza vikiburutwa huku wanafunzi wakinong`onezana na kutoka nje ya Darasa.**

6. MALAIKA: ***(akijisemesha)*** Kazi hii ni ngumu. Nitaweza kweli? Nitakufa mimi...!

7. DANIEL : Ooh, mbona umekasirika. Umekasirishwa na nini?

8. MALAIKA : Ahh… ni wewe Daniel! Umejuaje niko hapa?

9. DANIEL : Si chuo ni kimoja, na wahadhiri ni wale wale… Mimi ni mwanafunzi wa mwaka wa pili…. Nasomea masuala ya kilimo na uhandisi. Kuna tatizo lolote….Unaonekana una wasiwasi

10.MALAIKA : Hizi kazi ni nyingi na ngumu sana. Natia bidii kusoma lakini sioni nikifaulu.

11. DANIEL : Unakosea…!

12. MALAIKA: Unamaanisha nini?

13. DANIEL: Lazima uniruhusu nikusaidie au ujiunge na kikundi cha wanafunzi kusoma pamoja.

14. MALAIKA: Kikundi cha wanafunzi kusoma pamoja?

15. DANIEL: Wajua, wanafunzi wanapo kuwa na kikundi cha kusoma pamoja, hugawana majukumu, na hivyo kupunguza ule mzigo. Kila mwanafunzi hufanya utafiti wa mada aliyopewa, na kisha wanapokutana tena hubadilishana mawazo na kuambiana kuhusu utafiti waliofanya. Hii huwapunguzia mzigo na kujifunza mengi zaidi kuliko mtu kusoma peke yake.

16. MALAIKA: Asante sana! Huo ni msaada mkubwa kwangu. Lakini nitawezaje kujiunga na kikundi kama hiki?

17. DANIEL : Zungumza na wanafunzi wenzako darasani. Kumbuka, pia wao wana matatizo kama yako! Mbali na hayo,***(akijaribu kumtongoza)*** mimi pia naweza kukusaidia wakati wowote…! Ehhe, hebu nione unafanya nini?

18. **MTANGAZAJI:** Malaika sasa ameanza kujifunza mengi kutoka kwa rafiki wa dhati. Je atafaulu, au bado kunachangamoto nyingine?.

**MUZIKI**

***<u>SCENE 2: KATIKA BUSTANI NA CHUONI</u>***.

19. CINDY : Kwa hivyo unaona ulimwengu umekufikia ukingoni kwa kuwa umeanguka mtihani wako wa kwanza?

20.MALAIKA : Cindy, kwako wewe ni rahisi maana hujali, lakini mimi,…wewe huelewi!

21 CINDY : Kuelewa nini? Eti kwamba msichana mdogo wa miaka 19 kama wewe anakibeba mgongoni kijiji kizima?

22. MALAIKA: Nimeanguka mtihani Cindy…!

23. CINDY : Hapana, hukuanguka mtihani, umejaribu sana, hasa ikizingatiwa mazingira yanayokukabili. Una mengi sana ya kujifunza. Na tukizungumzia suala hilo la kujifunza… ehhe ..rafiki amefika.

24.MALAIKA: ***(wakinong´onezana)*** Cindy! si rafiki yangu.

25. CINDY : ***(kitefute)*** Habari Daniel..? Sawa basi tuonane baadaye Malaika!

26. DANIEL : Habari yako Cindy.. Habari Malaika?

27. MALAIKA: Kwani unanifuata?

28. DANIEL : Hata…., imetokea tu kwamba kila niendapo upo!. Waonaje tukienda sinema jioni?

29. MALAIKA: La, siwezi, nahitaji kusoma.

30. DANIEL : Unajaribu kukataa ombi langu … sivyo?

31. MALAIKA : Sahamani, hapa nimekuja kusoma sio kufanya urafiki wa kimapenzi.

32. DANIEL : Sawa basi tusahau ya sinema jioni, labda basi nikusaidie na kazi yako ya utafiti wa kilimo.

33. MALAIKA : Daniel !!???

***MUZIKI***

## SCENE 2: KATIKA MAKTABA

34. CINDY : (***akichakura vitabu na makaratasi)*** Hallo … Malaika… sssssccchh… Malaika unasoma nini?

35.SAUTI: SSSSHHHHHH…

36. CINDY : ***(kwa sauti kubwa)*** Malaika, nini mbaya?

37. VOICE : Kimya tafadhali!

38. CINDY: ***(Anavuta kiti. Anakaribia na huku akichakkarisha nguo zake.)***

39. MALAIKA : ***(akimnong´onezea)*** Ni ripoti ya karo na utaratibu wa gharama chuoni.

40 . CINDY : ***(akimnong´onezea)*** Ndio, unajua muhula huu unakaribia kufika ukingoni.. Sisi sote hupewa ripoti hiyo kuhusu akaunti zetu na karo tunayopasa kulipa muhula ujao. ..Ehhe, hebu sasa niambie, kuna mapya?

41. MALAIKA : Sasa nitapata wapi pesa hizi zote? Sidhani naweza kupata tena usaidizi kijijini, hawana tena kuku wa kunadi.

42. CINDY : ***(dhihaka***) Mnauza kuku kulipa karo? Basi lazima muwe munauza shehena za kuku hao!

43. MALAIKA : Si mzaha, Cindy!

44. CINDY : Sawa, wewe ni rafiki yangu na napasa kukusaidia niwezavyo. Nafikiri jambo la kwanza kabisa tunahitaji kumuona muhadhiri-mshauri wa wanafunzi.

45. MALAIKA : Anaweza kunisaidia?

46. CINDY : Kwanza chuo kitaelewa matatizo yako. Kisha tutatafuta ushauri. Labda chuo kinatoa msaada wa masomo kwa wanafunzi kutoka……si unaelewa namaanisha nini….

47. MALAIKA : … wanafunzi maskini ?

48. CINDY : Sijasema hiyo, napendelea kuwaita wanafunzi kutoka familia zisizojiweza. Sawa lakini kabla ya kutafuta ushauri, kwanza tuangalie katika mtandao wa intanet.

49. MALAIKA : Cindy, hebu sasa twende kumuona muhadhiri,… ni muhimu kwangu!

50. CINDY : Unafikiri kwanini nataka kuangalia mtandao wa Intaneti? Si mzaha.! Ni lazima tutafute ufadhili wa masomo, huwezi kujua, labda kunamashirika yanayotoa misaada ya masomo kwa wanafunzi wa kike, au wasichana wanaosomea taaluma zinazochukuliwa kuwa za wanaume pekee, au

hata masuala ya maendeleo ya kijamii na mengineyo…

51. MALAIKA : Cindy, kweli wewe ni rafiki wa dhati, lakini hebu niambie ulijuaje mambo yote haya?

52. CINDY : Jaribu kusoma magazeti mwenzangu, au tizama televisheni au hata kuuliza pia. Utajifunza mengi tu!

53. MALAIKA : Kichwa sasa chanizunguka.

54. CINDY : Tunahitaji kupata msaada wa masomo, hebu twende!

55. **MTANGAZAJI :** Malaika huenda anakosa usingizi kuhusu atakakopata karo ya muhula ujao,lakini kinachopasa kumpa wasi wasi zaidi ni ukosefu wa ufahamu kuhusu habari muhimu zinazoweza kumsaidia kupata msaada wa karo. Bado anajifunza na kisha kwa haraka zaidi.Je atafaulu kupata msaada wa masomo?

**MUZIKI**

## SCENE 3:CHUONI

SOUNDS: ***NDEGE WAKIIMBA, SAUTI ZA CHINI KWA CHINI ZA WANAFUNZI WAKIWA WANABARIZI:***

56. MALAIKA: Ohoo, Cindy, Unalo ujualo?, kuna Watu wengi wanatafuta msaada wa masomo. Na hali yangu ni ngumu sana. Kazi za shule, kutafuta karo,.. na macho yote ya kijiji yakiwa kwangu, Wanakijiji wanamatarajio makubwa sana kutoka kwangu na…..

57. CINDY : Usiweke mayai yako kwenye kapu moja. Endelea kutafuta huo ufadhili wa masomo na vile vile uwahimize wanakijiji kufanya mnada zaidi wa kuku *(acheka)* na pia utafute kazi ufanye wakati wako wa ziada.

58. MALAIKA: Nitafuta kazi? Siwezi kuacha masomo.

59. DANIEL : ***(akikaribia)*** Nani aache masomo?

60. CINDY/MALAIKA: Habari Daniel!

61. DANIEL: Habari zenu wasichana, kwanini munaonekana wanyonge hivi?

62. MALAIKA : Cindy anasema nitafute kazi nifanye ili nigharamie masomo yangu. Lakini nikifanya kazi nitasoma saa ngapi?

63. DANIEL : Si wazo baya. Unaweza kufanya kazi wakati wako wa ziada; bora tu kama unaweza kujipanga. Lakini isiwe kazi ya kuanzia saa 3 hadi saa 11. Inaweza kukupatia pato la kugharamia sehemu ya mahitaji yako.

64.CINDY : ***(akitafakari )*** Najua mtu anayeweza kukuajiri katika mkahawa mmoja hapa mjini.

65. MALAIKA: Kweli? Nani huyo ?

66. CINDY : Babangu. Hebu tumpigie simu.

67. DANIEL : Waona! Sasa naweza kukutembelea na kula chakula nikipendecha ..kuku na chips!

68. CINDY/MALAIKA : Daniel!!!!!

**MUZIKI**

## OUTRO

69.**MTANGAZAJI** Malaika sasa anajifunza mengi, sio tu taaluma yake ya kilimo na uhandisi bali pia jinsi ya kujimudu maishani akiwa mwanafunzi chuoni. Baadaye anafaulu kupata kazi katika mkahawa huo. Kinachosalia ni kumudu maisha ya kazi na masomo chuoni. Anafaulu baada ya kujikakamua . Na je maisha yatakuwaje kule kijijini? Ungana nasi kwa makala yajayo ya `Learning by Ear' tukizungumzia elimu na maisha ya Chuo kikuu. Unaweza pia kutembelea mtandao wetu www.dw-world.de/lbe ujifunze mengi kuhusu vipindi vya Learning by Ear Noa bongo jenga maisha yako. Kadhalika unaweza kututumia maoni yako kuhusu vipindi hivi. Hadi wakati mwengine kwa makala mengine, kwa heri.